
# Báb

## *Mtangulizi wa Siku Mpya*




**Báb alizaliwa 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, mji ulioko sehemu ya kusini mwa Iran. Alikuwa bado mtoto mdogo, wakati baba Yake alipofariki. Alilelewa na mjomba Wake, ambaye alimpeleka shule akiwa na umri mdogo.**




**Mwalimu wa Báb kwa haraka alitambua uwezo Wake mkubwa na aliona kwamba hakuwa na uwezo wa kumfundisha mtoto asiye wa kawaida kama huyo. Báb alijaliwa na Mungu elimu ya asili.**



**Wakati ule watu wa Iran walikuwa wakingojea ujio wa Mjumbe mpya wa Mungu. Walisali ili punde aweze kudhihirishwa, akileta kipindi cha amani na haki duniani. Wengi waliyaacha makazi yao kwenda kumtafuta Yule Mwahidiwa.**



**Mnamo 23 Mei 1844, kijana mmoja aliwasili huko Shíráz akimtafuta Yule Mwahidiwa. Báb alimkuta nje ya malango ya mji na akamwalika nyumbani Kwake kujipumzisha baada ya safari yake ndefu. Hapo Báb alitangaza kwamba Yeye Ndiye Yule Ambaye ujio Wake watu walikuwa wakingojea kwa shauku mno.**




**Neno “báb” maana yake lango au mlango. Báb alitangaza kwamba punde Mjumbe mwingine wa Mungu angetokea Ambaye angeunganisha watu wote wa ulimwengu kuwa familia moja. Báb alikuwa kama mlango ukiwaongoza wanadamu kuelekea wakati mpya na mtukufu ujao.**



**Idadi ya wafuasi wa Báb iliongezeka kwa haraka. Iran nzima, walianza kuenezo mafundisho matakatifu Aliyoyafunua.**




**Punde mamlaka za kiserikali na makasisi, ambao walikuwa wakihofia kupoteza madaraka yao, juu ya watu waliinuka dhidi ya Imani hii mpya ya Mungu. Walimfunga Báb katika ngome iliyokuwa sehemu ya mbali iliyojitenga ya nchi, mbali kabisa na wafuasi wake.**



**Wafuasi wa Báb walipata mateso ya kikatili sana. Walishambuliwa, kupigwa na kutupwa gerezani. Maelfu waliuawa, lakini Hoja ya Mungu iliendelea kuenea.**



**Mnamo 1850 Báb aliuawa kifo cha kishahidi. Kwa amri ya serikali, Yeye pamoja na mmoja wa wafuasi Wake walitundikwa uwanjani pamoja na kupigwa risasi na kikosi cha wanajeshi. Báb alikuwa na umri wa miaka 31 tu.**



**Báb aliyatoa maisha Yake ili kuandaa njia kwa ajili ya ujio wa Bahá’u’lláh, “Utukufu wa Mungu”, Ambaye bendera ya Imani Yake ya Imani ilikusudiwa kuinuliwa katika kila kona ya sayari.**

Hakimiliki © 2001, 2023 ya Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.2.PE Agosti 2025, zilizochapishwa katika kiswahili

Taasisi ya Ruhi
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org